



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na. MDC / I.20/21/77

01 Aprili, 2021

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa kazi ifuatayo:-

MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II: (Nafasi moja)

1. SIFA ZA MWOMBAJI:

Kuajiriwa wenye cheti cha kidato cha nne (IV) au sita (VI) wenye cheti cha Utunzaji Kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi.

KAZI NA MAJUKUMU YA MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II:

- Kutafuta kumbukumbu/ nyaraka/ mafaili yanayohitajiwa na wasomaji.
- Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka.
- Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (classification and boxing) kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
- Kuweka/kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki (file racks/cabinets) katika masjala/ vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.
- Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka nk.) katika mafaili.
- Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/ nyaraka kutoka Taasisi za Serikali.

2. MSHAHARA:


Cheo cha Msaidizi wa Kumbukumbu II kina mshahara wa TGS B kwa mwezi.

3. MASHARTI YA JUMLA:

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- Mwombaji ambaye ni mtumishi wa Umma apitishe maombi yake kwa mwajiri wake.
- Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.
- Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Elimu na Taaluma kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.
- "Testimonials", "Provisional Results" "Statements of results" nk. Hazitakubalika.
- Waombaji waweke picha moja katika barua zao za maombi.
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NECTA.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 14/04/2021 saa 9:30 Alasili.
- Barua zote zitumwe kwa anwani iliyopo hapo chini:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya Mbinga,
S.L.P. 194,
MBINGA.

NB: Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ambayo ni:- www.mbingadc.go.tz



Juma A. Mnwele
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MBINGA